CONTROLLED

TBS/QMD/PCERT/P05

**TANZANIA BUREAU OF STANDARDS**

**UTARATIBU WA KUPATA LESENI YA ALAMA YA UBORA NA CHETI CHA UBORA WA BIDHAA**

COPY NO: DG
REV/ ISSUE NO: 5

**JANUARI 2026**

## 1 UTANGULIZI

Mpango wa uthibitishaji wa ubora wa bidhaa umeandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) chini ya Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) kama mmiliki wa mpango. Mpango huu umejengwa katika msingi wa "Type 5 Scheme" uliobainishwa katika Kiwango ISO/IEC 17067, ukijumuisha kazi na shughuli zifuatazo:

**1.1** **Uchaguzi**, ukijumuisha mipango na maandalizi:

**a)** Kupokea maombi ya uthibitishaji wa bidhaa,
**b)** Kusaini makubaliano ya uthibitishaji wa bidhaa (mpango wa ukaguzi na upimaji),
**c)** Kuainisha kiwango cha bidhaa kwa maombi ya mteja husika,
**d)** Malipo ya ada za uthibitishaji ubora,
**e)** Kuwasilisha mpango wa tathmini kwa mteja.

**1.2** **Uamuzi**, unajumuisha:

**a)** Tathmini ya mchakato wa uzalishaji na ukaguzi wa vipengele vingine vya mfumo wa usimamizi wa mteja vinavyohusika moja kwa moja na usimamizi wa udhibiti wa ubora wa bidhaa, kupitia mapitio ya nyaraka na tathmini ya eneo husika;

**b)** Ukaguzi na upimaji wa bidhaa.

**1.3** **Mapitio**, yanajumuisha:

Kuchunguza ushahidi wa uzingatiaji wa matakwa uliopatikana wakati wa hatua ya uamuzi ili kubaini kama matakwa yaliyobainishwa yametimizwa.

**1.4** **Uamuzi kuhusu uthibitishaji wa ubora**, unajumuisha:

Kutoa, kudumisha, kupanua mawanda, kupunguza mawanda, kusitisha na kuondoa ithibati ya ubora.

**1.5** **Utoaji leseni**, unajumuisha:

**a)** Alama ya ubora,
**b)** Kutoa taarifa za waombaji/wamiliki wa leseni kwa umma,
**c)** Matumizi mabaya ya cheti na alama ya ubora.

**1.6** **Ufuatiliaji**, unajumuisha:

**a)** Ukaguzi na upimaji wa sampuli za bidhaa kutoka kiwandani na sokoni,
**b)** Tathmini ya mchakato wa uzalishaji.

## 2 MAWANDA

Mpango huu utatumika kwa bidhaa za aina zote.

## 3 KUSUDI LA MFUMO

Kusudi la mfumo huu ni kutoa kanuni ambazo zinapaswa kufuatwa katika uthibitishaji wa ubora wa aina zote za bidhaa. Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) itatoa huduma zake za uthibitishaji ubora kwa kuzingatia Kiwango cha ISO/IEC 17065 na matakwa ya mfumo huu. Wateja wa Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) watazingatia matakwa ya mfumo huu na ya Mkataba wa Uthibitishaji wa Bidhaa (Mfumo wa Ukaguzi na Upimaji) (TBS/QMD/PCERT/01/F04-005). Wateja pia watazingatia matakwa yoyote yatakayoainishwa na viwango husika vya bidhaa pamoja na matakwa yoyote ya kisheria.

## 4 MAHITAJI YA AWALI

### 4.1 Nyaraka za Kisheria za Maombi

Kila mteja atakayeomba uthibitisho wa bidhaa chini ya mpango huu atafanya hivyo kwa mujibu wa sheria na atapaswa kuwa na nyaraka zifuatazo:

a) Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN)
b) Leseni ya Biashara ya Kiwanda

Nyaraka nyingine zinazohusiana ni:

c) Muundo wa taasisi, ukijumuisha kitengo cha Udhibiti Ubora (QC) au Uhakikisho Ubora (QA)
d) Mpangilio wa eneo la kiwanda
e) Ramani ya jinsi ya kufika kiwandani
f) Mtiririko wa hatua za uzalishaji
g) Orodha ya malighafi na sehemu zinakotoka
h) Lebo ya bidhaa
i) Orodha ya michakato inayofanywa na wakandarasi kwa mkataba
j) Rasilimaliwatu na rasilimali za kiufundi (mfano: maabara, vifaa vya ukaguzi, n.k.)
k) Mwakilishi wa kiwanda wa kuwasiliana naye

## 4.2 Uthibitisho

Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) ya TBS ina haki ya kufanya uthibitisho wa uhalali wa nyaraka zozote zinazowasilishwa na mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa.

## 4.3 Uzingatiaji wa Matakwa

Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa atahakikisha kwamba anakidhi matakwa ya mpango wa uthibitishaji wa ubora wa bidhaa kabla ya kuwasilisha maombi ya huduma hiyo na baada ya kupewa leseni ya kutumia alama ya ubora au cheti cha ubora.

## 4.4 Ununuzi wa Kiwango

Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa atanunua kiwango cha bidhaa husika katika maktaba ya TBS au kwa kutuma maombi kupitia barua pepe info@tbs.go.tz au nambari ya bure ya huduma kwa wateja, **0800 110 827.**

## 4.5 Uwezo wa Wafanyakazi

Wafanyakazi wanaofanya kazi ya uthibitisho wa ubora katika asasi zenye leseni au vyeti vya ubora vya TBS watatakiwa kuwa na sifa zinazostahili kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao. Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) itakuwa na haki

ya kuthibitisha uwezo wa wafanyakazi hao kwa kukagua kumbukumbu za mafunzo stahiki waliyopewa pamoja na tathmini za utendaji wao.

## 4.6 Mfumo wa Ubora

Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa atatimiza matakwa yafuatayo ya msingi ya usimamizi wa ubora ikiwa mfumo wake wa ubora haujasajiliwa chini ya ISO 9001:

a) Udhibiti wa bidhaa zisizokidhi matakwa ya viwango,
b) Udhibiti wa vifaa vya ufuatiliaji na upimaji,
c) Udhibiti wa kumbukumbu na nyaraka,
d) Mpango wa ukaguzi wa ubora wa ndani (kutambua sehemu za ukaguzi na upimaji katika mchakato wa uzalishaji),
e) Kumbukumbu za ukaguzi wa ubora wa ndani,
f) Taratibu za kushughulikia malalamiko ya wateja na kumbukumbu zake,
g) Ratiba ya matengenezo ya mashine na kumbukumbu zake,
h) Taratibu za ufuatiliaji na urudishaji wa bidhaa.

## 4.7 Shughuli za Udhibiti wa Mchakato wa Uzalishaji

Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa ataandaa na kuhifadhi nyaraka za uzalishaji zinazobainisha mchakato wa uzalishaji. Nyaraka hizo pia zitabainisha vipengele vinavyopimwa katika maeneo na hatua mbalimbali za upimaji na ukaguzi, ikiwa ni pamoja na ukaguzi au upimaji wa mwisho wa bidhaa kabla ya usafirishaji, kama ifuatavyo:

### i) Malighafi inayoingia

Malighafi yote inayoingia kwenye mchakato inapaswa kuthibitishwa ili kuhakikisha inakidhi viwango husika. Malighafi kama vile viambato vinavyotumika kuhifadhi na kuzuia bidhaa kuharibika haraka zitapaswa kuwa na vyeti vya ubora au nyaraka zinazoonyesha kuwa zinakidhi viwango, kanuni, au mahitaji ya matumizi.

### ii) Udhibiti wa uzalishaji

Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa atakuwa na vyombo vya ufuatiliaji na upimaji vilivyoainishwa katika kiwango husika cha bidhaa, au kuthibitisha kuwa atavipata vyombo hivyo atakapohitaji kutekeleza matakwa haya. Vyombo hivyo vinapaswa kuwa na vyeti au ripoti sahihi za ugezi ambazo zimehifadhiwa. Mwombaji wa huduma atahakikisha unakuwepo ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa katika mchakato mzima wa uzalishaji.

**iii) Ukaguzi wa bidhaa ya mwisho**

Bidhaa zilizokamilika zitakaguliwa ili kuthibitisha kuwa zinakidhi matakwa yote ya kiwango husika cha bidhaa. Kumbukumbu za ukaguzi huu zitahifadhiwa.

## 4.8 Ada za Uthibitishaji wa Ubora

Wakati wa mchakato wa uthibitishaji wa ubora wa bidhaa, mteja atalazimika kulipa ada ya tathmini ya kiwanda, gharama za upimaji, na ada ya kila mwaka ya uthibitishaji wa ubora, kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Viwango (Ada na Tozo), zinazopatikana kwenye tovuti ya TBS: www.tbs.go.tz.

## 4.9 Mchakato Wa Uthibitishaji Wa Ubora

### 4.9.1. Maombi ya Uthibitishaji wa Ubora

a) Mwombaji wa huduma ya uthibitishaji wa ubora wa bidhaa atazingatia mchakato wa kupata leseni/cheti, kama ulivyobainishwa katika utaratibu huu.

b) Fomu ya maombi ya kielektroniki inayopatikana katika mfumo wa i-SQMT wa TBS itajazwa na kuwasilishwa pamoja na taarifa zinazohitajika katika hatua ya uchunguzi, ambazo zinajumuisha yafuatayo:

   i) Jina la bidhaa inayotakiwa kuthibitishwa (au majina kama bidhaa ni zaidi ya moja),

ii) Kiwango au nyaraka nyingine zenye maainisho zitakazotumika kwa uthibitishaji ubora,

iii) Taarifa za jumla za mteja, ikiwa ni pamoja na jina na anuani ya eneo lake kijiografia,

iv) Shughuli za mteja (shughuli, majukumu, au michakato maalum inayofanywa kama sehemu ya uzalishaji), rasilimali watu, rasilimali za kiufundi, jinsi mteja anavyosimamia na kuhakikisha kuwa wakandarasi wanazingatia ubora katika utendaji wao wa kazi kulingana na masharti ya mikataba yao (ikiwa anao), na matakwa ya kisheria kama yalivyobainishwa katika Kifungu 4.1.

c) Mkataba wa Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (TBS/QMD/PCERT/01/F04-005) utakamilishwa baada ya kutimizwa kwa mahitaji ya maombi ya uthibitishaji wa ubora.

d) Mkaguzi aliyepangiwa kiwanda husika atatayarisha mpango kwa ajili ya tathmini ya kiwanda kama inavyohitajika na kiwango husika cha bidhaa.

### 4.9.2. Tathmini

#### i) Tathmini ya Kiwanda

a) Tathmini ya kiwanda itafanyika katika eneo la kiwanda. Tathmini hii itajumuisha ukaguzi wa eneo, shughuli za udhibiti wa mchakato wa uzalishaji kama ilivyoainishwa katika Kifungu 4.7 uthibitisho wa mfumo wa usimamizi wa ubora wa bidhaa wa mteja, ukaguzi wa nyaraka za mteja, na ukaguzi wa kuthibitisha iwapo bidhaa zinakidhi matakwa ya ubora.

b) Mkaguzi atatumia mpango wa tathmini (TBS/QMD/PCERT/01/F02-004) na orodha ya mambo ya kuzingatia anapokwenda kufanya tathmini ya kiwanda.

c) Uchukuaji wa sampuli kwa ajili ya upimaji wa maabara utafanyika wakati uzalishaji ukiendelea, kama ilivyobainishwa katika kiwango cha bidhaa husika.

d) Baada ya shughuli za tathmini kukamilika, mkaguzi atakusanya taarifa na ushahidi uliokusanywa wakati wa tathmini ya kiwanda na kuwasilisha kwa Meneja wa Uthibitishaji Ubora wa Bidhaa/Meneja wa Kanda ambaye atamteua afisa uthibitishaji ubora kwa ajili ya mapitio.

**ii) Upimaji**

Bidhaa zitakaguliwa na kupimwa kulingana na vigezo vilivyobainishwa katika kiwango husika.

### 4.9.3. Mapitio

a) Afisa wa uthibitishaji ubora ambaye hakuhusika katika mchakato wa tathmini atapitia matokeo ya tathmini.

b) Maandalizi ya leseni yatafanyika endapo matokeo ya tathmini yatakidhi matakwa husika.

c) Mteja ataarifiwa kuchukua hatua za marekebisho endapo matokeo ya tathmini hayatakidhi matakwa.

### 4.9.4. Uamuzi wa Uthibitishaji Ubora

Mchakato wa uamuzi wa uthibitishaji wa bidhaa utaanzishwa baada ya masharti yote ya uthibitishaji ubora kutimizwa. Wateja wote wataarifiwa mara moja kupitia mfumo wa kielektroniki kuhusu uamuzi uliotolewa na hatua za marekebisho zinazohitajika. Baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa hatua za marekebisho kutoka kwa mteja, mkaguzi atatumwa kwa ajili ya kuthibitisha kurekebishwa kwa mapungufu yaliyobainishwa wakati wa tathmini ya kiwanda na/au kuchukua sampuli upya kwa ajili ya kupima tena. Baada ya hatua hiyo, mchakato huendelea kwa kuzingatia utaratibu uliobainishwa katika kifungu cha 4.9.2 hadi 4.9.3.

### 4.9.5. Nyaraka za Uthibitishaji Ubora

a) Leseni/cheti na nyaraka zake husika ambazo ni "Facsimile" (TBS/QMD/PCERT/01/F04-006) na Jedwali A (TBS/QMD/PCERT/01/F04-003) zinabeba taarifa zote kuhusu jina na anuani ya Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB), tarehe ya kuthibitishwa, jina na anuani ya mteja, aina ya bidhaa, jina la chapa ya bidhaa, tarehe ya mwisho wa leseni/cheti, kiwango kilichotumika na wajibu wa TBS na mteja.

b) Leseni/cheti halisi cha TBS hubeba saini ya Mkurugenzi Mkuu, muhuri wa TBS na alama ya kielektroniki.

c) Hakuna nyaraka rasmi za uthibitishaji wa ubora wa bidhaa zitakazotolewa kwa mteja kabla uamuzi wa kutoa au kupanua wigo wa leseni/cheti haujafanyika, masharti ya uthibitishaji ubora kutimizwa na makubaliano ya uthibitishaji ubora kukamilishwa/kusainiwa.

d) Leseni/cheti kitakachotolewa kitakuwa halali kwa kipindi cha mwaka mmoja. Leseni/cheti kitahuishwa kila mwaka baada ya kufanyika kwa tathmini mpya ya bidhaa ili kuona kama bado inakidhi matakwa ya kiwango.

## 5 MAHITAJI YA BAADA

### 5.1 Matumizi ya Leseni, Cheti na Udhibiti wa Alama ya Ubora ya "tbs"

Mkataba wa Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (TBS/QMD/PCERT/01/F04-005) uliokamilika utatumika, sanjari na masharti yafuatayo:

a) Mteja anaweza kutangaza kuwa ubora wa bidhaa yake umethibitishwa na kutumia leseni au cheti chake kama ushahidi.

b) Mteja hatatoa taarifa za uongo au za kupotosha kuhusu aina, hadhi au mawanda ya leseni au cheti cha ubora.

c) Mteja atazingatia kwa umakini matumizi ya alama ya ubora ya "tbs" kama inavyosimamiwa na Kifungu cha 18 cha Sheria ya Viwango, Sura ya 130, Kanuni ya 3 ya Kanuni za Viwango (Usajili wa Maeneo na Uthibitishaji wa Ubora wa

Bidhaa) za mwaka 2021, pamoja na Jedwali A la Mkataba wa Leseni (TBS/QMD/PCERT/01/F04-003).

d) Mteja ataiwekea alama ya ubora ya "tbs" bidhaa iliyopewa leseni ya ubora kwa kuzingatia "facsimile" (TBS/QMD/PCERT/01/F04-006); na maneno "APPROVED BY TBS TPC No." kwa bidhaa iliyopewa cheti cha ubora.

e) Alama ya ubora itatumika tu kwa bidhaa zinazozalishwa kwenye eneo ambako sampuli za bidhaa zilichukuliwa kwa ajili ya ukaguzi na upimaji, ambalo liko ndani ya mawanda ya leseni au cheti cha ubora, kama ilivyobainishwa kwenye leseni au cheti husika.

## 5.2 Orodha ya Bidhaa Zilizothibitishwa

Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) ina mfumo wa kielektroniki (iSQMT) wenye orodha ya bidhaa zilizothibitishwa, na taarifa hizo hutolewa kwa umma kupitia jarida la mara mbili kwa mwaka lijulikanalo kama *Announcer* pamoja na tovuti rasmi ya TBS, www.tbs.go.tz.

## 5.3 Shughuli za Ufuatiliaji

a) Ufuatiliaji kiwandani na kwenye masoko utafanyika angalau mara mbili kwa mwaka wa uhai wa leseni/cheti. Uhai wa leseni/cheti ni pamoja na uzingatiaji wa masharti ya Mkataba wa Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (TBS/QMD/PCERT/01/F04-005), yanayobainisha wajibu wa mmiliki wa leseni na Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB).

b) Sampuli za bidhaa zilizothibitishwa ubora zitachukuliwa kutoka kiwandani na sokoni ili kuhakikisha utekelezaji endelevu wa matakwa ya uthibitisho wa ubora wa bidhaa.

c) Hakutakuwa na taarifa ya awali kwa mteja kuhusu ziara za ufuatiliaji. Iwapo wakati wa ziara kutabainika kutokuzingatiwa kwa masharti ya leseni au cheti, mmiliki wa leseni/cheti atatakiwa kuchukua hatua za kurekebisha.

d) Ufuatiliaji wa soko pia hufanyika pale ambapo kuna malalamiko kuhusu bidhaa zilizothibitishwa. Kila mara uchunguzi kama huo unapofanyika, mzalishaji atapewa nakala ya matokeo ya uchunguzi huo. Wazalishaji watapaswa kuweka wazi masoko yao ili kuwezesha ufuatiliaji wa bidhaa zao. Pale ambapo dosari zitabainika sokoni, mteja atapaswa kuchukua hatua za kurekebisha dosari hizo, ambazo zinaweza kuhusisha kurejesha bidhaa au kuchukua bidhaa iliyo na kasoro na kuibadilisha na bidhaa mpya au inayokidhi viwango.

## 5.4 Bidhaa Zisizokidhi Viwango

Mmiliki wa leseni/cheti atakuwa na utaratibu utakaomwezesha kufuatilia bidhaa na kuondoa bidhaa zisizotimiza masharti ya uthibitisho wa ubora.

## 5.5 Kusitishwa, Kupunguzwa, Kusimamishwa na Kufutwa kwa Uthibitisho

Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) ina haki ya kusitisha, kupunguza, kusimamisha au kufuta uthibitisho wa ubora chini ya masharti ya Mkataba wa Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (TBS/QMD/PCERT/01/F04-005).

## 5.6 Kurejeshwa kwa Leseni Iliyosimamishwa

Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) inaweza kurejesha leseni iliyosimamishwa iwapo itapokea maombi kutoka kwa mteja pamoja na ushahidi wa utekelezaji wa hatua za kurekebisha kasoro zilizosababisha kusimamishwa kwa leseni husika.

## 5.7 Malalamiko na Rufaa

i) Malalamiko na rufaa zote zinazohusiana na uthibitisho wa ubora wa bidhaa zitatatuliwa kwa mujibu wa utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa za wateja (TBS/QMD/PCERT/P02), na mlalamikaji ataarifiwa juu ya matokeo ya uchunguzi.

ii) Baada ya kupokea malalamiko rasmi au rufaa inayohusiana na uthibitisho wa ubora wa bidhaa, Mamlaka ya Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa (PCB) itakiri

kupokea malalamiko/rufaa hiyo kupitia barua, barua pepe au mfumo wa kielektroniki (i-SQMT) na kumtaarifu mteja ipasavyo.

iii) Kazi ya kushughulikia malalamiko au rufaa itafanywa na watumishi ambao hawakuhusika katika shughuli za uthibitisho wa ubora wa bidhaa zinazohusiana na malalamiko au rufaa husika.

iv) Wateja waliowasilisha malalamiko au rufaa wataarifiwa juu ya matokeo ya uchunguzi kupitia barua, barua pepe au mfumo wa kielektroniki (i-SQMT).

v) Mteja yeyote asiyeridhishwa na uamuzi wowote wa Shirika unaohusiana na uthibitisho wa ubora wa bidhaa anaweza kukata rufaa kwa Waziri anayehusika na Viwanda na Biashara ndani ya siku kumi na nne.

## 5.8 Upatikanaji wa Mpango

Mpango huu wa Uthibitishaji wa Ubora wa Bidhaa utapatikana kwa wadau wote wanaouhitaji kupitia tovuti ya TBS, www.tbs.go.tz.